



U SADI NA DAWAH: NJIA MBILI, MWISHO MBILI



noor.gallery



● **Kwa jina la Allah Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu** ●

وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ
يَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَيُقِيمُونَ
الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَيُطِيعُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ
أُولَئِكَ سَيَرْحَمُهُمُ اللَّهُ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٧١﴾
[التوبة: ٧١]

*Na Waumini wanaume na Waumini wanawake ni
marafiki (wa kusaidiana na kuungana mkono katika
kheri) wao kwa wao. Wanaamrisha mema na
wanakataza maovu na wanasimamisha Swala na
wanatoa Zaka na wanamtii Allah na Mtume wake.
Hao Allah atawashushia rehema. Hakika, Allah ni
Mwenye nguvu mno, Mwenye hekima sana*

Qurani (9:71)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



﴿الْمُنْفِقُونَ وَالْمُنْفِقَاتُ بَعْضُهُمْ مِّنْ بَعْضٍ
يَأْمُرُونَ بِالْمُنْكَرِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمَعْرُوفِ
وَيَقْبِضُونَ أَيْدِيَهُمْ نَسُوا اللَّهَ فَنَسِيَهُمْ إِنَّ
الْمُنْفِقِينَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٦٧﴾﴾

[التوبة: ٦٧]

Wanafiki wanaume na wanafiki wanawake; wote ni hali moja (wanafanana katika unafiki na kutoamini). Wanaamrisha maovu na wanakataza mema na wanakunja mikono yao (kwa kukataa kutoa katika njia za heri). Wamemsahau Allah, basi naye amejifanya amewasahau (amewaacha na unafiki wao). Hakika, wanafiki ndio waovu hasa

Qurani (9:67)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



قُلْ هَذِهِ سَبِيلِي أَدْعُو إِلَى اللَّهِ عَلَى
بَصِيرَةٍ أَنَا وَمَنِ اتَّبَعَنِي وَسُبْحَانَ اللَّهِ
وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٠٨﴾

[سورة يوسف: ١٠٨]

**Sema: Hii ndiyo njia yangu; ninalingania
(ninahubiri) kwa Allah kwa kujua, mimi na
wanaonifuata. Na Allah ametakasika na
mimi siomiongoni mwa washirikina**

Qurani (12:108)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



هَافَلُولَا كَان مِّنَ الْقُرُونِ مِن قَبْلِكُمْ أُولُوا بَقِيَّةٍ يَنْهَوْنَ
عَنِ الْفَسَادِ فِي الْأَرْضِ إِلَّا قَلِيلًا مِّمَّنْ أَنْجَيْنَا مِنْهُمْ وَاتَّبَعَ
الَّذِينَ ظَلَمُوا مَا أُتْرِفُوا فِيهِ وَكَانُوا مُجْرِمِينَ ﴿١١٦﴾ وَمَا كَانَ
رَبُّكَ لِيُهْلِكَ الْقُرَىٰ بِظُلْمٍ وَأَهْلِهَا مُصْلِحُونَ ﴿١١٧﴾

[هود: ١١٦-١١٧]

*Na lau ingekuwepo katika karine za kabla yenu masalia ya
watu wa kheri wanakataza maovu ardhini, (lakini
hawakuwepo miongoni mwa watu wa kheri) isipokuwa
wachache tu. Miongoni mwa (walioamini) tuliowaokoa kutoka
kwenye adhabu. Na wale waliodhulumu wakafuata starehe
zao walizoneemeshwa, na wakawa waovu Na hakuwa Mola
wako mlezi ni mwenye kuangamiza watu wa miji kwa dhulma
tu na hali watu wake ni watenda mema*

Qurani (11:116-117)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



﴿وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ خَلِيفَةً ۖ
قَالُوا أَتَجْعَلُ فِيهَا مَنْ يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ الدِّمَاءَ وَنَحْنُ
نُسَبِّحُ بِحَمْدِكَ وَنُقَدِّسُ لَكَ ۖ قَالَ إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٠﴾﴾

[سورة البقرة: ٣٠]

*Na (kumbuka) Mola wako alipowaambia
Malaika kuwa: Kwa yakini, mimi
nitamuweka Khalifa ardhini. Wakasema:
Hivi unamuweka humo atakayefanya
uharibifu humo na kumwaga damu, na
wakati sisi tunakutakasa kwa kukusifu?
(Allah) Akasema: Mimi ninajua msichokijua*

Qurani (2: 30)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



فَهَزَمُوهُمْ بِإِذْنِ اللَّهِ وَقَتَلَ دَاوُودُ جَالُوتَ وَءَاتَاهُ
اللَّهُ الْمُلْكَ وَالْحِكْمَةَ وَعَلَّمَهُ مِمَّا يَشَاءُ وَلَوْلَا دَفْعُ
اللَّهُ النَّاسَ بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لَفَسَدَتِ الْأَرْضُ
وَلَكِنَّ اللَّهَ ذُو فَضْلٍ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٢٥١﴾

[سورة البقرة: ٢٥١]

Basi waliwashinda kwa idhini ya Allah na Daudi akamuua Jaluti, na Allah akampa (Daudi) ufalme na utume na akamfundisha aliyoyataka. Na kama Allah asingewakinga watu baadhi yao kwa wengine, bila shaka ardhi ingeliharibika, lakini Allah ni Mwenye hisani kubwa mno kwa walimwengu

Qurani (2:251)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



﴿وَالْوِاسْتِقَامُوا عَلَى الطَّرِيقَةِ لَأَسْقِينَاهُمْ مَاءً
غَدَقًا ﴿١٦﴾ لِنَفْتِنَهُمْ فِيهِ وَمَنْ يُعْرِضْ عَنْ ذِكْرِ رَبِّهِ
يَسْلُكْهُ عَذَابًا صَعَدًا﴾ ﴿١٧﴾

[الجن: ١٦-١٧]

(Allah Anasema): Kwamba lau wangelinyooka na wakasimama sawasawa kwenye njia, bila shaka Tungeli wanyweshaji maji kwa wingi ili tuwatie katika majaribio kwayo. Na anayepuuza Ukumbusho wa Mola wake, Atamsukuma kwenye adhabu ngumu

Qurani (72: 16-17)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



﴿وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْقُرَىٰ ءَامَنُوا وَاتَّقَوْا لَفَتَحْنَا
عَلَيْهِمْ بَرَكَاتٍ مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ وَلَٰكِن
كَذَّبُوا فَأَخَذْنَاهُم بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ﴾ ٩٦

[الأعراف: ٩٦]

Na lau kama watu wa miji wameamini na
kumcha Allah tungewafungulia baraka
nyingi kutoka mbinguni na ardhini na lakini
wamekadhibisha kwa sababu hiyo
tumewashikisha adabu kwa sababu ya yale
waliyokuwa wanayachuma (wanayafanya)

Qurani (7: 96)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّينِ قَدْ تَبَيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيِّ فَمَنْ
يَكْفُرْ بِالطَّاغُوتِ وَيُؤْمِنْ بِاللَّهِ فَقَدْ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ
الْوُثْقَى لَا انْفِصَامَ لَهَا وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٥٦﴾

[البقرة ٢٥٦]

Hakuna kulazimisha (watu kuingia) katika dini. Hakika, uongofu umekwishajitenga na upotovu. Basi anayemkataa Twaghuti na kumuamini Allah, bila shaka yeye ameshika kishikio madhubuti kisichovunjika. Na Allah ni Mwenye kusikia sana, Mjuzi sana

Qurani (2:256)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA



هُرَوَلُوْ شَاءَ رَبُّكَ لَأَمْنٌ مِّنْ فِي الْأَرْضِ كُلُّهُمْ جَمِيْعًا
أَفَأَنْتَ تُكْرِهُ النَّاسَ حَتَّى يَكُونُوا مُؤْمِنِيْنَ ﴿٩٩﴾

[سورة يونس 99]

Na lau kama Mola wako Mlezi angetaka,
basi kwa hakika kabisa, wote waliomo
duniani wangeamini. Hivi, wewe
unawalazimisha watu ili wawe
waumini?

Qurani (10: 99)

MWINGILIANO WA AIKON - BONYEZA

